Tangazo la Serikali Na…….la terehe ………………

**SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA**

**(SURA YA 290)**

**SHERIA NDOGO**

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 7 na 13*

SHERIA NDOGO ZA (**ADA NA USHURU**) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA, 2023

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (**Ada na Ushuru**) za Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba, 2023, na zitaanza kutumika baada ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali | *Jina na tarehe ya kuanza kutumika* |
| 2. | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba | *Eneo la Matumizi* |
| 3. | Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale ambapo imeelezwa vinginevyo, maneno yafuatayo yatakuwa na maana iliyoelezwa mbele yake:<br><br>*"**Ada**"* maana yake ni malipo yanayotozwa na Halmashauri kwa mtu yeyote anayeomba kibali ama ridhaa ya Halmashauri ya kufanya shughuli yoyote ambayo kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi inastahili kulipiwa ada<br><br>*"**Afisa Muidhinishwa**"* maana yake ni mtumishi yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa na Mkurugenzi kutekeleza Sheria Ndogo hizi<br><br>*"**Bidhaa**"* maana yake ni kitu chochote kinachouzwa sokoni, gulioni, mnadani, dukani au sehemu nyingine yoyote iliyoruhusiwa<br><br>*"**Halmashauri**"* maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba<br><br>*"**Huduma**"* maana yake ni shughuli zote zinazotolewa na Halmashauri, au namtu mwingine yeyote, ambazo zinapaswa kulipiwa ada kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi<br><br>*"**Lori la mizigo**"* maana yake ni gari lolote lenye uzito kuanzia tani 3.5 na, ambalo hufanya kazi za kubeba mizigo, ikiwa ni pamoja na madini | *Fasili maalum ya maneno yaliyotumika* |

| | | |
|---|---|---|
| | ya ujenzi katika eneo la Halmashauri<br><br>*“**Madini ya ujenzi**”* ni pamoja na mchanga, kokoto, changarawe, mawe, kifusi na maliasili zingine za namna hiyo ambazo kwa kawaida hutumiwa kwa ujenzi katika eneo la Halmashauri<br><br>*“**Mazao mchanganyiko**”* maana yake ni mazao yote yanayotokana na shughuli za kilimo, isipokuwa korosho<br><br>*“**Mifugo**”* maana yake itajumuisha ng’ombe, mbuzi, kondoo, kuku na aina yoyote nyingine ya wanyama ambao kwa kawaida hufugwa katika eneo la Halmashauri<br><br>*“**Mkurugenzi**”* maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba, au Afisa yeyote wa Halmashauru anayekaimu nafasi hiyo<br><br>*“**Mnada**”* maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuuzia na/au kununulia mifugo<br><br>*“**Mnunuzi**”* maana yake ni mtu binafsi, taasisi au kikundi cha watu kinachojishughulisha na ununuzi wa mazao au mifugo<br><br>*“**Muuzaji**”* maana yake ni mtu binafsi, taasisi au kikundi cha watu kinachojishughulisha na uuzaji wa mazao au mifugo<br><br>*“**Soko**”* ni sehemu au eneo maalum lililotengwa kwa ajili ya shughuli za kuuza na kununua bidhaa na mazao mbalimbali.<br><br>*“**Ushuru**”* maana yake ni fedha zote ambazo Halmashauri itatoza kwa mazao na mifugo iliyouzwa katika masoko, magulio, minada na machinjio | |
| 4. | (1) Halmashauri itatoza ada na/au ushuru kwa ajili ya huduma au bidhaa zinazotolewa kwa malipo katika eneo lake, huduma hizo zikijumuisha utoaji wa vibali na leseni mbalimbali kama inavyoonyeshwa katika nyongeza ya Sheria Ndogo hizi<br><br>(2) Ada na ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya kutolewa kwa huduma husika au vinginevyo kama itakavyoamriwa na kuelekezwa na Mkurugenzi kwa maandishi | *Malipo ya ada/ushuru* |
| 5. | Mtu yeyote anayewajibika kulipa ada ama ushuru atalipa ada ama ushuru huo kabla ya kupata au kutoa huduma kwa kiasi na utaratibu unaotajwa katika Sheria Ndogo hizi | *Wajibu wa kulipa ada/ushuru* |

| | | |
|---|---|---|
| 6. | (1) Kila mmiliki wa pikipiki za magurudumu mawili au matatu na inayofanya biashara ya kusafirisha abiria, atawajibika kuandikisha pikipiki hiyo, ambapo;<br><br>(a) pikipiki hiyo itakuwa na kibao cheupe cha namba ya usajili<br><br>(b) pikipiki hiyo itabandikwa alama na namba maalum ambayo itatolewa na Halmashauri baada ya kulipiwa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi<br><br>(2) Mtu yeyote anayeendesha pikipiki ya kusafirishia abiria, pamoja na kuheshimu masharti mengine ya Sheria ya Usalama barabarani pia atawajibika kuhakikisha kwamba anavaa sare maalum inayomtambulisha kama dereva wa pikipiki ya abiria<br><br>(3) Halmashauri itatoza ushuru kwa ajili ya pikipiki na teksi zote zinazofanya biashara katika eneo lake<br><br>(4) Ushuru wa pikipiki na teksi utakadiriwa kwa kila siku, na utalipwa kwa mwaka, ambapo mlipaji atawajibika kuwa amelipa ushuru wake wa mwaka kila ifikapo tarehe 25 ya mwezi Julai ya mwaka wa fedha unaohusika | *Ushuru wa pikipiki* |
| 8 | (1) Halmashauri itatoza ushuru wa maegesho kwa malori yote ya mizigo yanayofanya kazi katika eneo lake<br><br>(2) Kila mmiliki wa lori la mizigo atawajibika kulipia na kupewa kibali kinachoruhusu lori lake kufanya kazi katika eneo la Halmashauri<br><br>(3) Ushuru wa kibali cha lori la kusafirishia mizigo utalipwa kama unavyotajwa katika nyongeza ya Sheria Ndogo hizi | *Ushuru wa malori ya mizigo* |
| 9 | Halmashauri itatoza ushuru kwa magari yote yanayoingia katika stendi kuu ya mabasi kwa namna na kiasi kilichotajwa katika nyongeza ya Sheria Ndogo hizi | *Ushuru wa Stendi* |
| 10 | (1) Halmashauri itatoza kodi ya vibanda vyote vinavyopatikana katika masoko yake kwa mujibu wa nyongeza ya Sheria Ndogo hizi<br>(2) Ni marufuku kwa mpangaji yeyote wa kibanda kinachomilikiwa na Halmashauri kupangisha kibanda hicho kwa mtu mwingine bila kwanza kupata ridhaa ya maandishi ya Mkurugenzi au Afisa muidhinishwa<br>(3) Halmashauri itakuwa na haki ya kuingia na kukagua usafi, uimara na/au usalama wa kibanda cha biashara wakati wowote katika muda wa kazi, ilimradi kuingia huko kusiathiri mtumiaji wa kibanda au wateja | *Kodi ya vibanda vya biashara* |

| | | |
|---|---|---|
| | wake | |
| 11. | (1) Halmashauri inaanzisha utaratibu wa kutoza ushuru wa mazao mchanganyiko yatakayouzwa katika vyama ya ushirika vya msingi ambavyo vitateuliwa na kutangazwa na Mkurugenzi<br><br>(2) Ushuru wa mazao yote mchanganyiko utatozwa kwa kiasi cha **3%** ya bei ya kuuzia, na utalipwa na mnunuzi mara baada ya kulipa fedha za muuzaji, na kabla ya kusafirisha mazao yaliyonunuliwa<br><br>(3) Mara baada ya kulipa ushuru wa mazao chini ya Sheria Ndogo hizi, mnunuzi atakuwa na haki ya kudai na kupewa stakabadhi kwa malipo aliyofanya, na stakabadhi hiyo itasomwa kwa pamoja na kibali cha kusafirishia mazao kitakachotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi | *Ushuru wa mazao mchanganyiko* |
| 12. | Ni marufuku kwa mtu yeyote kusafirisha mazao mchanganyiko kutoka sehemu moja kwenda nyingine ndani ya eneo la Halmashauri, isipokuwa kwa utaratibu unaotajwa katika Sheria ndogo hizi:<br><br>(a) kama ni mnunuzi awe amelipia kibali cha kununua mazao kinachotajwa katika nyongeza ya Sheria ndogo hizi, na awe na stakabadhi inayoonyesha kwamba amelipia ushuru unaostahili<br><br>(b) mazao yasafirishwe kwa gari la mizigo lililoidhinishwa na kutambuliwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi<br><br>(c) kama ni mkulima awe na barua au kibali cha Afisa Mtendaji wa Kijiji alikolimia mazao husika, kinachoonyesha kwamba mazao hayo yanasafirishwa na mkulima mwenyewe kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa ajili ya kuyahifadhi ama kuyauza | *Usafirishaji wa mazao* |
| 13. | (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutoa matangazo ya namna yoyote bila kupata kibali cha Mkurugenzi au Afisa muidhinishwa<br><br>(2) Matangazo yanayotolewa na taasisi za kidini, vyama vya siasa, mashirika yasiyo ya kiserikali au taasisi yoyote ambayo shughuli zake si za kibiashara hayatatozwa ada ya matangazo<br><br>(3) Ada ya matangazo itatozwa kwa kuzingatia utaratibu na viwango vinavyotajwa katika nyongeza ya Sheria Ndogo hizi<br><br>(4) Mtu yeyote anayetaka kutoa matangazo ya sauti katika muda unaozidi saa 12.30 jioni atazingatia utaratibu wa ziada ambao ataelekezwa na Afisa muidhinishwa | *Ada ya matangazo* |

| | | |
|---|---|---|
| | | |
| 14. | (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuanzisha ama kuendeleza shughuli za kuendesha ukumbi wa disko, sinema ama maonyesho bila kupata kibali kutoka ofisi ya Mkurugenzi<br><br>(2) Mtu yeyote anayetaka kuanzisha ama kuendeleza ukumbi na/au shughuli za kupiga disko, kuonyesha sinema, muziki hai au maonyesho atawasilisha maombi kwa Mkurugenzi kwa kutumia fomu iliyoambatanishwa katika nyongeza ya Sheria Ndogo hizi, na atawajibika kulipa ada kama inavyoonyeshwa katika nyongeza ya Sheria Ndogo hizi | *Vibali vya kupiga disko, kuonyesha sinema, muziki hai na maonyesho* |
| 15. | (1) Kunaanzishwa utaratibu wa kusajili vikundi vyote vya shughuli za sanaa katika eneo la Halmashauri<br><br>(2) Kikundi chochote kinachotaka kusajiliwa kitawasilisha maombi yake kwa Mkurugenzi kwa njia ya maandishi, kikieleza aina ya sanaa inayohusika, anuani kamili ya makazi, orodha ya wanachama na anuni zao, na Mkurugenzi au Afisa mudhiniwa, akisharidhika kwamba kikundi hicho kimekidhi vigezo vya usajili atasajili kikundi hicho<br><br>(3) Kabla ya usajili, kikundi kilichopitishwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kitalipa ada ya usajili kama inavyoonyeshwa katika nyongeza ya Sheria Ndogo hizi | *Ada ya shughuli za kiutamaduni* |
| 16. | Huduma zifuatazo, ambazo hutolewa na mabaraza ya Kata zitatozwa ada kama inavyoonyeshwa katika nyongeza ya Sheria Ndogo hizi:<br><br>(a) kuandikisha shauri la madai<br>(b) kupatiwa nakala ya hati ya usuluhishi wa mgogro<br>(c) kudurusu jalada | *Ada ya huduma za mabaraza ya Kata* |
| 17. | (1) Halmashauri itakodisha ukumbi wake, viti na vifaa vingine kama inavyoonyeshwa katika nyongeza ya Sheria ndogo hizi<br><br>(2) Mkazi yeyote atakuwa na haki ya kuomba, na akishakubaliwa ataweza kupitia nyaraka za wazi za Halmashauri, hasa zile zinazohusu vikao vya wazi au taarifa zingine za wazi, na mtu yeyote atakayeruhusiwa kufanya hivyo atawajibika kulipa ada ya huduma hiyo kwa kiasi na utaratibu iliotajwa katika nyongeza ya | *Ada ya kukodi ukumbi na vifaa vingine ya Halmashauri* |

| | | |
|---|---|---|
| | Sheria Ndogo hizi | |
| 18. | Huduma za machinjio zitatozwa ada kwa kiasi na utaratibu unaotajwa katika nyongeza ya Sheria Ndogo hizi | *Ada ya machinjio* |
| 19. | Halmashauri itatoza ushuru kwa minara yote ya simu iliyomo katika eneo lake, na ushuru huo hautaathiri mkataba utakaofungwa baina ya kampuni ya simu inayohusika na mmiliki wa eneo la shamba au kiwanja ambako mnara huo umejengwa | *Ushuru wa minara ya simu* |
| 20. | Ni marufuku kwa mtu yeyote kujenga, ama kuendeleza kwa namna yoyote, kiwanja katika eneo lililopimwa bila kwanza kupata kibali cha ujenzi kilichotolewa na Halmashauri | *Mambo ambayo yanapigwa marufuku* |
| 21. | (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba madini ya ujenzi katika maeneo ambayo hayaruhusiwi. Machimbo ya madini ya ujenzi hayatafanywa na mtu yeyote, isipokuwa kama mtu huyo;<br>(a) amepata kibali cha kufanya hivyo, ambacho kitatolewa na Halmashauri baada ya kulipwa kwa ada kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi<br>(b) ametoa taarifa ya kuchimba madini ya ujenzi katika mamlaka ya kijiji kinachohusika<br>(c) hadaiwi fedha zozote ambazo zilistahili kulipwa kwa Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi<br>(2) Halmashauri ya Kijiji italipwa 40% ya ushuru wa madini ya ujenzi yanayochimbwa katika eneo lake | |
| 22. | (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kubandika bango la matangazo ya biashara katika eneo lolote la Halmashauri, au kutoa matangazo ya biashara kwa sauti isipokuwa kwa utaratibu unaotajwa katika Sheria Ndogo hizi<br>(2) Mtu yeyote atakayetaka kuweka bango la matangazo ya biashara katika eneo lolote atahakikisha kwamba kabla ya kuweka bango hilo:<br>(a) Amepata ridhaa ya mmiliki wa eneo hilo<br>(b) Amelipa ada inayostahili kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi<br>(c) Bango hilo haliko katika eneo la hifadhi ya barabara | |

| | | |
|---|---|---|
| 23. | Mtu yeyote atakayekiuka au kwenda kinyume na kifungu chochote cha Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki Mbili (**200,000.00**) na isiyozidi Shilingi Milioni Moja **(1,000,000.00)** au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote faini na kifungo kwa pamoja. | *Adhabu* |
| 24. | Sheria Ndogo hizi zinafuta Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba za mwaka 2011 | |

## NYONGEZA YA KWANZA

SEHEMU A

| *Na.* | *Shughuli inayohusisha kibali/leseni* | *Ada/Ushuru* |
|---|---|---|
| 1. | Kibali cha kuendesha biashara ya kuonyesha sinema/video kwa mwaka | (a) 20,000/= mjini<br>(b) 10,000/= vijijini |
| 2. | Kibali cha kuendesha biashara ya kupiga disko/muziki hai, kuonyesha maigizo, sarakasi, mieleka, ngumi, kunyanyua vyuma, vichekesho, taarab na jazi, kwa siku moja | 5,000/= |
| 3. | Ushuru wa biashara ya kusafirisha abiria kwa pikipiki kwa mwaka mmoja | 50,000/= |
| 4. | Ushuru wa minara ya simu kwa mwaka | 2,000,000/= |
| 5. | Ada ya kuandikisha/kuendesha kikundi cha sanaa kwa mwaka | 20,000/= |
| 6. | Kibali cha kusafirisha mazao | 10,000/= |
| 7. | Kibali cha kutumia skimu ya umwagiliaji kwa mwaka | 200,000/= |
| 8. | Ada ya utunzaji skimu | 40,000/= |
| 9. | Ada ya Kibali cha uvuvi | 20,000/= |
| 10. | Ada ya michezo ya bahati nasibu (*betting*) | 20,000/= kwa mwezi |
| 11. | Ada ya michezo ya kubahatisha (bonanza) | 300,000/= kwa mwaka |

SEHEMU B

| *Na.* | *Ada ya malori ya mizigo na ushuru wa magari yanayoingia stendi* | |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya lori la mizigo kwa siku | 2,000/= |
| 2. | Ushuru wa stendi kwa basi dogo la abiria kwa siku | 2,000/= |
| 3. | Ushuru wa stendi kwa basi kubwa la abiria kwa siku | 3,000/= |
| 4. | Ushuru wa stendi kwa gari dogo la mizigo lisilolipiwa ada ya mwaka, kwa siku | 2,000/= |

SEHEMU C

| Na. | *Ada ya kulaza magari na mitambo isiyo ya serikali katika yadi ya Halmashauri* | |
|---|---|---|
| 1. | Magari madogo ya watu binafsi, kwa usiku mmoja | 1,000/= |
| 2. | Magari makubwa ya abiria na mizigo, kwa usiku mmoja | 3,500/= |
| 3. | Mashine na/au mitambo ya ujenzi wa barabara/visima kwa siku | 5,000/= |
| 4. | Pikipiki | 500/= |

SEHEMU D

| Na. | *Ada ya matangazo kwa njia ya mabango na sauti* | |
|---|---|---|
| 1. | Mabango ya biashara yasiyong'ara (kwa kila futi moja ya mraba) kwa mwaka | 15,000/= |
| 2. | Mabango ya biashara yanayong'ara (kwa kilafuti moja ya mraba) kwa mwaka | 25,000/= |
| 3. | Mabango ya biashara yasiyong'ara (yanayodumu kwa hadi siku 7) | 3,000/= |
| 4. | Mabango ya biashara yanayong'ara (yanayodumu kwa hadi siku 7) | 4,500/= |
| 5. | Mabango ya biashara yasiyong'ara (yanayodumu kwa hadi siku 30) | 5,000/= |
| 6. | Mabango ya biashara yanayong'ara (yanayodumu kwa hadi siku 30) | 7,500/= |
| 7. | Matangazo ya biashara kwa sauti, kwa siku moja | 5,000/= |

SEHEMU E

| Na. | *Ada ya huduma za machinjio na ukaguzi wa nyama machinjioni* | |
|---|---|---|
| 1. | Ukaguzi wa nyama ya ng'ombe | 5,000/= |
| 2. | Ukaguzi wa nyama ya mbuzi | 3,000/= |
| 3. | Ukaguzi wa nyama ya kondoo | 3,000/= |
| 4. | Ushuru wa kulaza ng'ombe machinjioni | 1,000/= |
| 5. | Ushuru wa kulaza mbuzi machinjioni | 500/= |

| | | |
|---|---|---|
| 6. | Ushuru wa kulaza kondoo machinjioni | 500/= |
| 7. | Ushuru wa kuingiza ng’ombe kwaajili ya uchinjaji | 1,000/= |
| 8. | Ushuru wa kuingiza mbuzi kwaajili ya kuchinjwa | 500 |
| 9. | Ushuru wa kuingiza kondoo kwaajili ya kuchinjwa | 500 |
| 10. | Ushuru wa kuingiza samaki kwaajili ya kuuzwa | 1,000/= kwa tenga moja |

SEHEMU F

| *Na.* | *Ushuru wa watoa huduma wadogowadogo* | |
|---|---|---|
| 1. | Mafundi seremala, kwa mwaka | 10,000/= |
| 2. | Watengenezaji wa vifaa na watoa huduma ya umeme kwa mwaka | 10,000/= |
| 3. | Gereji za magari | 20,000/= |
| 4. | Gereji za pikipiki | 10,000/= |
| 5. | Kutengeneza na kukodisha baiskeli | 5,000/= |
| 6. | Mafundi cherehani | 7,000/= |

SEHEMU G

| *Na.* | *Ada na Ushuru wa biashara mbalimbali* | |
|---|---|---|
| 1. | Meza ya biashara ndani ya soko, kwa mwaka | 20,000/= |
| 2. | Meza ya biashara nje ya soko, kwa mwaka | 10,000/= |
| 3. | Mabanda (kiosks) kwa mwaka | 10,000/= |
| 4. | Mabanda ya kuuzia kuku kwa mwezi | 5,000/= |
| 5. | Wauza urembo kwa mwezi | 5,000/= |
| 6. | Vibanda vya matunda kwa mwezi | 5,000/= |

SEHEMU H

| *Na.* | *Ada ya ukaguzi na idhini ya ujenzi* | |
|---|---|---|
| 1. | Minara ya simu (telecom towers) | 40,000/= |
| 2. | Jengo lenye urefu wa kuanzia ghorofa mbili | 50,000/= |
| 3. | Nyumba za kulala wageni | 30,000/= |
| 4. | Kituo cha Mafuta | 250,000/= |
| 5. | Nyumba ya makazi na biashara zinginezo | 20,000/= |
| 6. | Majengo ya taasisi zisizo za kiserikali | 30,000/= |
| 7. | Maghala ya kuhifadhia mazao na bohari zingine | 100,000/= |
| 8. | Uzio uliojengwa kwa matofali | 10,000/= |

SEHEMU I

| *Na.* | *Ada ya kubadilisha ramani ya jengo lililopo (alteration fee)* | |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba ya kuishi | 20,000/= |
| 2. | Nyumba ya biashara | 30,000/= |
| 3. | Bohari, kiwanda, ghala la kuhifadhia mazao, nk | 50,000/= |

SEHEMU J

| *Na.* | *Uchangiaji wa mfuko wa upimaji* | |
|---|---|---|
| 1. | Kiwanja kidogo (high density) | 5,000/= |
| 2. | Kiwanja cha kati (medium density | 7,000/= |
| 3. | Kiwanja kikubwa (low density) | 10,000/= |

SEHEMU K

| *Na.* | *Huduma za Baraza la Kata* | *Ada* |
|---|---|---|
| 1. | Kuandikisha shauri la madai | 10,000/= |
| 2. | Kupata nakala ya hati ya usuluhishi | 5,000/= |
| 3. | Kudurusu jalada | 10,000/= |

SEHEMU L

| *Na.* | *Ada ya kutumia mali za Halmashauri* | |
|---|---|---|
| 1. | Kukodi ukumbi kwa siku moja | 250,000/= |
| 2. | Kukodi gari la mizigo kwa siku moja, bila mafuta | 300,000/= |
| 3. | Kukodi viti kwa siku moja, kwa kiti | 500/= |
| 4. | Kukodi vipaza sauti na matarumbeta kwa siku moja | 50,000/ |
| 5. | Kutumia uwanja wa michezo kwa shughuli za kibiashara kwa siku moja | 20,000/= |
| 6. | Kusoma nyaraka za wazi za Halmashauri kwa siku | 2,000/= |
| 7. | Kutumia maktaba ya Halmashauri kwa siku | 2,000/= |

SEHEMU M

| *Na.* | *Ushuru wa Madini ya Ujenzi* | |
|---|---|---|
| 1. | Lori la mchanga, kokoto au changarawe chini ya tani 7 kwa tripu | 15,000/= |
| 2. | Lori la mchanga, kokoto au changarawe la tani 7 kwa tripu | 25,000/= |
| 3. | Lori la mawe chini ya tani 7 | 25,000/= |
| 4. | Lori la mawe la tani 7 | 30,000/= |

SEHEMU N

| *Na* | *Ada ya maegesho katika eneo la Hospitali* | *Kwa siku* |
|---|---|---|
| 1. | Baiskeli | 500/= |
| 2. | Pikipiki | 1000/= |
| 3. | Bajaj | 2000/= |
| 4. | Gari lolote la mtu binafsi | 100/= |
| 25. | Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba imetiwa katika Sheria Ndogo hizi, katika kikao chake cha Baraza la Madiwani kilichoketi leo tarehe……..mwezi……….. mwaka 2023 mbele ya wafuataoː<br><br>…………………………………<br><br>**MARIAM SAID MWANZALIMA**<br><br>MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA<br><br>TANDAHIMBA<br><br>NA<br><br>……………………………….<br>**BAISA ABDALLAH BAISA**<br>MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA<br><br>TANDAHIMBA<br><br>**…………………………………….**<br>**ANGELLAH JASMINE KAIRUKI (MB)**<br>**WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS**<br>**(TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITA)**<br>**Dodoma,**<br>**Julai, 2023** | Lakiri ya Halmashauri |